



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MADINI

UONGEZAJI THAMANI MADINI,
BIASHARA YA MADINI NA MASOKO



UONGEZAJI THAMANI MADINI

“Dhamira ya Serikali ni kujenga na kuendeleza Viwanda vya ndani na kuongeza Mapato ya Serikali kutoka Sekta ya Madini.”

- Wizara imefanya uhamasishaji kwa wawekezaji hadi kufikia mwaka 2024 takribani viwanda 14 vya uongezaji thamani madini vimejengwa katika maeneo mbalimbali nchini. Viwanda hivi vinajihusisha na usafishaji wa dhahabu kwa kiwango cha 99.99 kabla ya kusafirishwa nje ya nchi, ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria ya Madini Sura ya 123 ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake .
- Wizara ya Madini imendelea na marekebisho ya sheria inayowataka wazalishaji, wafanyabiashara na Wachimbaji wa madini ya dhahabu kutenga asilimia 20 ya uzalishaji wa madini kusafishwa katika viwanda nchini na kuuzwa ndani ya nchi.
- Wizara ya Madini imeendelea kuhakikisha madini yote ya viwandani na ujenzi yanaongezewa thamani hapa nchini. Madini kama Kaolin, Quartz, Clay, Feldspar, Magnetite, Limestone, Dolomite Gypsum, Bauxite, Pozzolana na Red soil. Serikali imeweka mkakati pia wa kuhakikisha jasi ngumu inaongezewa thamani hapa nchini ili kutengeneza plaster of paris, building plaster na chaki.
- Wizara inaendelea kuboresha Kituo cha Tanzania Gemological Centre (TGC) kwa lengo la kutekeleza Sera ya Madini ya Mwaka 2009 kuhusu Uongezaji Thamani Madini. Chuo hiki hutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ya vito katika fani za:-
Ukataji na ung'arishaji madini ya vito (Lapidary),

BIASHARA YA MADINI

“ Lengo la Wizara ni kuona shughuli za uchimbaji madini zinam-nufaisha mchimbaji kwa kupata kipato kitakachoinua maisha yao huku pia ikichangia katika uchumi wa nchi kwa kulipa kodi stahiki na hatimaye kuongeza Pato la Taifa.”

- Kifungu cha 18 (1) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kinakataza mtu kuwa na madini au kuuza madini isipokuwa kama ana leseni ya madini, leseni kubwa ya biashara ya madini (Dealer's Licence) au leseni ndogo ya biashara ya madini (Broker's Licence). Pia mwajiriwa, wakala au mkan-darasi wa mwenye leseni ataruhusiwa kuwa na madini kwa niaba ya wami-liku wa leseni za madini na leseni za biashara za madini.

- Kifungu cha Sheria ya Madini 18 (3) kinakataza mtu yeyote kusafirisha madini nje ya nchi bila kuwa na leseni ya uchimbaji madini, uchenjuaji wa madini, usafishaji wa madini, utafutaji wa madini au leseni kubwa ya biashara ya madini (Dealer's Licence).

Madini yanaruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi baada ya kulipiwa mrabaha husika na kuthaminiwa na Maafisa kutoka Tume ya Madini kwa kushirikisha vyombo vya Ulinzi na Usalama.

- Kwa mujibu wa kifungu 18 (4), yeyote atakayesafirisha madini nje ya nchi bila kuwa na leseni husika inayoruhusu kufanya hivyo au kutokulipa mrabaha anatenda kosa na akipatikana na hatia; atalipia faini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi (10,000,000) au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu (3) au adhabu zote kwa pamoja. Ikiwa kosa limetendwa na Kampuni adhabu yake ni kifungo kisichozidi Shilingi Milioni Hamsini (50,000,000).

AINA YA LESENI ZA BIASHARA YA MADINI

Kuna leseni za aina mbili za biashara ya madini

- 1) Leseni ndogo ya biashara ya madini (Broker's Licence)
- 2) leseni kubwa ya biashara ya madini (Dealer's Licence)

Waombaji wa leseni za biashara za madini ya vito (dealer licence) hutakiwa kuwa na mashine za kukata na kung'arisha madini kama ifuatavyo:-

- 1) Kwa leseni zinazomilikwa na watanzania mashine zisizopungua tano na
- 2) Kwa leseni zenye ubia na wageni mashine zisizopungua 30.

Utekelezaji wa takwa hilo la kisheria umepelekea kuwa na viwanda vya ukataji madini ya vito hapa nchini.

Wizara inaendelea kuhakikisha wachimbaji wa madini ya viwandani kama wanauza madini hayo kwenye viwanda vya saruji, vigae (tiles) na chupa kwa bei ambazo zitapelekea uchimbaji kuwa endelevu pamoja na viwanda hivyo.

VIWANDA VYA KUSAFISHA MADINI NCHINI

Serikali kupitia Wizara ya Madini imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kusafisha madini nchini. Viwanda hivyo vimejengwa katika mikoa ya Geita, Mwanza, Shinyanga, Dodoma na Dar es Salaam vyenye uwezo wa kusafisha kilo 1,210 za dhahabu kwa siku.



UREJESHWAJI MINADA NA MAONESHO YA MADINI YA VITO NCHINI

Wizara ya Madini inaendelea na mpango wake wa kurejesha minada ya madini ya vito ndani na nje ya nchi na kurejesha maonesho ya Kimataifa ya madini ya vito. Minada hiyo inatarajiwa kuanza baada ya Marekebisho ya Sheria ya Madini itakayowezesha utekelezaji wa urejeshwaji wa minada hiyo sambamba na mwongozo wa uendeshwaji wa minada kukamilika.

